**Sherehe za CCM zatikisa upinzani ..Uk.2**

tanzaniabora @tanzaniabora @tanzaniabora

# Tanzania BORA

Ni Mimi na Wewe

Tovuti: www.tanzaniabora.co.tz | ISSN 4256-1873 Toleo Na.19 Tanzania Bora IJUMAA Februari 07, 2025 Bei Tsh. 1,000 | Ksh. 100




# Chadema wajichimbia Bagamoyo kuikwepa CCM

>> Wadaiwa kuhofia shamra shamra za CCM Dodoma

>> Walifanya hivyo pia wakati wa Mkutano Mkuu

>> Timu ya wagombea Urais CCM yawakatisha tamaa

HABARI UK.2






## DART kutumia tikezi za kielektroniki

NA MWANDISHI WETU

WAKALA wa Mabasi Yaendayo Haraka DART umesema kuanzia mwezi Machi mwaka huu wa 2025 utasitisha rasmi matumizi ya tiketi za karatasi katika usafiri wa Mabasi Yaendayo Haraka na badala yake watumiaji wote wa Mabasi watatakiwa kutumia kadi janja ambazo zinaendelea kuuzwa katika vituo vikuu vya mradi huo.

Akizungumza Jijini Dar es Salaam wakati wa kuhitimisha mradi wa Maendelezo Yatokanayo na uboreshaji wa usafiri wa umma (TOD), Mtendaji Mkuu wa

Inaendelea Uk. 2



# Waziri mkuu ampa 5 Dkt. Samia kuipaisha Tanzania kimataifa

HABARI UK.2

# CHADEMA WAJICHIMBIA BAGAMOYO KUIKWEPA CCM

NA MWANDISHI WETU

UNAUKUMBUKA ule Mkutano Mkuu Maalum wa CCM uliofanyika jijini Dodoma Januari 18 na 19, ambao ulitoka na jina la Makamu Mwenyekiti wa CCM bara, Mzee Steven Wassira na kisha siku ya pili ukaibua majina ya wagombea Urais wa chama hicho Tanzania Bara, ambapo Dkt Samia alipitisha na Dkt Mwinyi akiridhiwa kupeperusha bendera katika uchaguzi huo kisiwani Zanzibar na Dkt Emmanue Nchimbi akateuliwa kuwa Mgombea mwenza wa Urais? basi tukio hilo lilikitesa sana chama cha upinzani Chadema.

Chama hicho kiliamua kupiga hesabu ili kupisha shamrashamra zile za CCM zipite ili wafanye jambo lao la Uchaguzi Mkuu, ndipo wakaamua kuiweka tarehe 21 Januari wakijua cha,ma hicho tawala kitakuwa kimemaliza mkutano wake pamoja na shamra sgamra ambazo kama wasingefanya hivyo zingezima tukio lal kwa nguvu zote.

Hatimauye wakafanya uchaguzi na aliyekuwa Mwenyekiti wake Freeman Mbowe akasalimu amri akiangushwa na Makamu wake Tundu Lissu.

Baada ya kumalizika uchaguzi huo ikachukua muda mtrefu kabla ya Mwenyekiti mpya hajahudhuria katika ofisi za chama hicho zilizopo Mikocheni hadi zilipopita shamra shamra za CCM ndipo naye akapiga hodi ofisini na kusikika akilegeza msimamo wake akiwataka wanachama wote hata wale waliodaiwa kuwa ni waasi ndani chama warejee ili kujipoanga upya.

Juzi Jumatano Kamati kuu ya (CHADEMA) ilikutana katika Hoteli ya Millenium wilayani Bagamoyo, safari hii wakipanga kufanya kikao chao siku moja kabla ya sherehe za CCM zilizofanyika jijini Dodoma, nia ikiwa ni kuhofia kutotulia vizuri kutokana na shamra shamra hizo kufuatiliwa karibu kila kona ya nchi na hata baadhi ya nchi za nje.

Hali hii inaonyesha jinsi chama hicho kinachotishwa na kivuli cha CCM na kiukifanya kipange mambo yake kwa kuangalia kalenda ya matukio ya chama kingine hali inayoonyesha hofu kubwa inayowasumbua kila uchao.



# WAZIRI MKUU AMPA 5 DKT. SAMIA KUIPAISHA TANZANIA KIMATAIFA

NA MWANDISHI WETU

WAZIRI MKUU wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Kassim Majaliwa amesema, Serikali itahakikisha inajiimarisha katika kukuza uchumi wake kwa kutumia rasilimali zilizopo ili kuweza kumudu kutekeleza maeneo yote muhimu.

Ameyasema hayo jana Februari 6, 2025 alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Mbozi George Mwanisongole, katika kipindi cha maswali kwa Waziri Mkuu Bungeni jijini Dodoma.

Mwanisongole alitaka kujua endapo Serikali imejiandaa vipi na mabadiliko ya sera za nje ya nchi ya Marekani ambayo yanaweza kuathiri utekelezaji wa sera za Elimu, Afya na Uchumi hususan miradi ya maendeleo inayofadhiliwa USAID.

Akijibu swali hilo Waziri Mkuu alise, kuwa Tanzania ina Uwezo wa Maliasili, kinachotakiwa ni Watanzania kushirikiana kuhakikisha tunatumia Maliasili na Rasilimali tulizonazo ili kujenga uchumi wa ndani na kuwezesha mipango na bajeti iweze kutekelezeka.

Alisema kuwa Tanzania inaheshimu sera za mambo ya nje na inatekeleza mikataba kwa mujibu wa sera hizo kama ilivyokubaliana na nchi husika katika maeneo mbalimbali. ”Tumeanza kuona nchi zenye uwezo mkubwa ikiwemo Marekani ikibadilisha sera zao na mabadiliko yake yanathiri baadhi ya nchi, kwetu sisi ni muhimu kuzingatia sera za nje na kuzitekeleza kama tulivyokubaliana.”

Pia, Waziri Mkuu ametumia fursa hiyo kumpongeza Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuendelea kuifanya Tanzania kuwa na mahusiano na nchi nyingi duniani na Marekani ni moja kati ya nchi hizo.

Wakati huo huo, Waziri Mkuu ameiagiza Wizara ya Kilimo iendelee kutoa elimu kuhusu uendeshwaji wa mfumo wa stakabadhi ghalani katika maeneo yote ambayo wanataka mazao yauzwe kwa kupitia mfumo huo ili kuondoa migogoro kwa wakulima.

Ametoa agizo hilo wakati akijibu swali la Mbunge wa Sumve, Kasalali Mageni aliyetaka kufahamu kauli ya Serikali kuhusu taharuki iliyojitokeza baada ya mazao ya choroko kuwekwa katika mfumo wa stakabadhi gharani kwa kuwa zao hilo ni chanzo cha chakula na akiba.

Waziri Mkuu amesema kwenye sekta ya kilimo yapo mazao ya biashara na chakula, pia yapo mazao ya chakula yanatumika kwa biashara, Serikali imeendelea kuimarisha masoko ya mazao kwa kutumia mifumo mbalimbali kufanya biashara za mazao hayo zikiwemo choroko.

Hata hivyo, Waziri Mkuu amesema anatambua yapo baadhi ya maeneo ambayo yana migogoro inayowafanya wakulima washindwe kuamini mfumo huo, hivyo ameiagiza Wizara ya Kilimo kuendelea kutoa elimu kwa wakulima ili kuondoa taharuki.

Alisema choroko ni miongoni mwa mazao ambayo Serikali imekuwa ikiratibu biashara yake pale ambapo mwananchi ameamua kutumia kama zao la kibiashara kupitia mifumo ya mauzo iliyopo kama kilimo cha mkataba au kuuza mkulima kuuza ndani na nje ya nchi.

Waziri Mkuu aliuzungumzia mfumo ambao sasa unatumika kwa mazao mengi kuuzwa kwa minada na inatakiwa iende vizuri, “tuliona tutumie mfumo wa stakabadhi ghalani ambao unawezesha wakulima kupata faida kubwa kutokana na ushindani wa wanunuzi unaofanyika kwa njia ya mnada.”

## SHEREHE ZA CCM ZATIKISA UPINZANI

NA MWANDISHI WETU

IKIWA imepita siku moja tu imepita tangu Chama Cha Mapinduzi CCM kilipofanya sherehe kubwa za kutimiza miaka 48,, katika Uwanja wa Jamhuri jijini Dodoma upoenda wa upinzani ni kama vile wamemwagiwa maji ya baridi.

Kuanzia juzi Februari 5, hadi hii leo hakuna kiongozi wa chama cha upinzani aliyekuwa tayari kuzungumzia hisia zake baada ya kushuhudia sherehe hizo, pia kusikiliza hotuba ya viongoizi mbalimbali na hasa mgeni rasmi Mwenyekiti wa CCM na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt Samia Suluhu Hassan.

Gazeti hili lilitaka kujua kauli za viongozi wa vyama vya upinzani, baada ya kufanyika kwa sherehe za CCM, lakini hakuna chama kilichokubali kutoa ushirikiako huku baadhi ya viongozi wakitoa kauli za hasira wakitaka wasiulizwe masuala yanayohusu chama kingine.

Uchunguzi wa gazeti hili umebaini kwamba sababu za msingi zilizowarudisha nyuma wapinzani ni pamoja na mikakati ya chama hicho tawala hasa safu ya viongozi imara waliosimamishwa na chama hicho kwa ajili ya kugombea nafasi za Urais Tanzania Bara, Mgombea Mwenza na Rais wa Ranzibar.

Kukubalika kwa Dkt Samia Rais wa Awamu ya Sita, Uzoefu wa Dkt Emmanuel Nchini ambaye si mgeni katika mizazi ya siasa za Tanzania pamoja na Dkyt Mwinyi anayetamba Zanzibar kwa kuinua uchumi hususan muundo mpya wa Uchumi wa Bluu, amekuwa ni kiongozi anayetarajiwa kukifikisha kisiwa hicho katika nchi ya ahadi.

Ukisikiliza kauli za Mwenyekiti wa Chadema Tundu Lissu hivi karibuni akionyesha nia ya kuwarudisha baadhi ya wanachama waliodaiwa kuasi baada ya kuingia bungeni bila kufuata taratibu, ilionekana wazi alitaka chama chake kiweke nguvu kugombea nafasi za Ubungu, hii inatokana na kuiona nafasi finyu ya kupata mgombea anayeweza kusimama dhidi ya mgombea wa CCM Dkt Samia.

Lakini baada ya hotuba ya jana ya Mwenyekiti wa CCM Dk Samia j0.Baada ya Viongozi wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema) kujifungia Bagamoyo kwa ‘fungate’ ya uponyaji majeraha ya kampeni za Uchaguzi wao uliofanyika tarehe 21 Januari 2025 , leo wameketi Kikao cha Kamati Kuu katika Hoteli ya Millenium wilayani Bagamoyo .ijini Dodoma hasa akisisitiza kuleta wanachama wanaokubalika ili kugombea nafasi za Ubunge na madiwani nao ukawa ni msumari mwingine kwa vyama vya upinzani ambao katika uchaguzi uliopita wa Serikali za Mitaa uliofanyika Mwezi Agosti mwaka jana na hata Uchaguzi Mkuu ulipita nao waliangukia pua.

# Prince Rahim kumrithi Aga Khan

NA MWANDISHI WETU

JUMUIYA ya Waislamu wa Kisheia Ismaili imemtangaza Prince Rahim Aga Khan V kama Imamu wa 50 wa urithi wa Waislamu wa Kisheia Ismaili, kufuatia kifo cha baba yake Aga Khan IV, aliyefariki dunia mjini Lisbon akiwa na umri wa miaka 88.

Mpito huu unaendeleza ahadi ya kudumu ya Imamu wa Ismaili kwa maendeleo ya kibinadamu, ambayo imekuwa nguzo muhimu ya kazi iliyofanywa chini ya uongozi wa Aga Khan IV ambaye katika uongozi wake wa miongo kadhaa, alijitolea kuboresha hali ya maisha duniani kote, kwa msisitizo maalum barani Afrika, Asia, na maeneo mengine yanayohitaji miradi ya maendeleo.

Kupitia Mtandao wa Maendeleo wa Aga Khan (AKDN), aliongoza upanuzi wa miradi inayolenga kuimarisha elimu, huduma za afya, maendeleo ya uchumi, na uhifadhi wa utamaduni katika mabara mbalimbali Afrika, hususan Tanzania, Kenya, Uganda, na Msumbiji, imekuwa eneo la kipaumbele kwa uwekezaji mkubwa katika shule, vyuo vikuu, hospitali, huduma za kifedha, na maendeleo endelevu yanayolenga kuleta mabadiliko ya muda mrefu.

Dira ya Kuendeleza na Kupanua Miradi

Chini ya uongozi wa Aga Khan V, Imamu wa Ismaili amethibitisha dhamira yake ya kuhakikisha kuwa miradi na programu zote zilizoanzishwa na Aga Khan IV zinaendelea na kuimarishwa zaidi.

"Kwa muda mrefu, Prince Rahim Aga Khan V amehusika kikamilifu katika uongozi wa AKDN, akiwa na mchango mkubwa katika mipango ya kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi, uhifadhi wa mazingira, na kupunguza umaskini".

Uwepo wa AKDN nchini Tanzania na Afrika kwa ujumla unasalia kuwa sehemu kuu ya dhamira yake, kupitia miradi inayoendelea ambayo inajumuisha:

Kuongeza upatikanaji wa elimu bora kupitia Shule za Aga Khan na vyuo vikuu vya Aga Khan Afrika Mashariki, kuimarisha mifumo ya afya na kuhakikisha upatikanaji wa huduma za kisasa za tiba kupitia Aga Khan Health Services (AKHS).

Miradi mingine ni kuhamasisha maendeleo ya uchumi kwa kusaidia ujasiriamali na miradi ya kifedha kupitia Mfuko wa Maendeleo wa Aga Khan (AKFED) na kuimarisha uendelevu wa mazingira, kwa kuendeleza miundombinu rafiki kwa mazingira na programu za kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi.

Jumuiya ya Ismaili inaposherehekea urithi wa Aga Khan IV, Imamat inaingia katika enzi mpya ya uongozi, ikiendeleza ahadi yake ya kuimarisha maendeleo ya kijamii, ustawi wa binadamu, na maendeleo endelevu kwa jamii zinazoihitaji zaidi.

Prince Rahim Aga Khan V ni mtoto wa kwanza wa Aga Khan IV, Amezaliwa tarehe 12 Oktoba 1971, amesoma katika Phillips Academy Andover na Chuo Kikuu cha Brown, na amehudumu katika bodi mbalimbali za AKDN, akiongoza pia Kamati ya Mazingira na Tabianchi, kwa kuhakikisha kuwa miradi ya maendeleo inaendana na malengo ya uendelevu wa muda mrefu.

# Majibu Wizara ya afya yamfurahisha Dkt. Tulia

NA MWANDISHI WETU

SPIKA wa Bunge, Mhe. Tulia Ackson, amekubali uwezo wa kitaalamu wa Wizara ya Afya baada ya Naibu Waziri wa Afya, Dkt. Godwin Mollel, kutoa majibu ya kina kuhusu matumizi ya teknolojia ya CRISPR-Cas9 katika matibabu ya magonjwa ya Seli mundu.

Katika majibu yake ya swali la nyongeza lililoulizwa na Mbunge wa Jimbo la Kawe, Mhe. Askofu Josephat Gwajima aliyehoji wizara imejiandaaje kuleta muswada Bungeni ili kuleta sheria maalum itakayoongoza watu waofanyiwa Gene Editing, Dkt. Mollel ameeleza jinsi teknolojia ya CRISPR-Cas9 inavyoweza kufanya uhariri wa jeni (gene editing) kwa usahihi mkubwa b

ila kuathiri maeneo mengine ya mwili. Amefafanua kuwa teknolojia hii ni ya kisasa na inatarajiwa kuwa na mchango mkubwa katika kutibu magonjwa ya kurithi, yakiwemo magonjwa ya seli mundu.



# DART KUTUMIA TIKEZI ZA KIELEKTRONIK

NA MWANDISHI WETU

WAKALA wa Mabasi Yaendayo Haraka DART umesema kuanzia mwezi Machi mwaka huu wa 2025 utasitisha rasmi matumizi ya tiketi za karatasi katika usafiri wa Mabasi Yaendayo Haraka na badala yake watumiaji wote wa Mabasi watatakiwa kutumia kadi janja ambazo zinaendelea kuuzwa katika vituo vikuu vya mradi huo.

Akizungumza Jijini Dar es Salaam wakati wa kuhitimisha mradi wa Maendelezo Yatokanayo na uboreshaji wa usafiri wa umma (TOD), Mtendaji Mkuu wa DART Dkt. Athumani Kihamia amesema ifikapo tarehe mosi mwezi Machi matumizi ya tiketi za karatasi katika kulipia nauli za mwendokasi yatasitishwa.

"Ni kweli tumeendelea kusisitiza watumiaji wa Mabasi yetu ya Mwedokasi wajitahidi kuwa na kadi janja na kuzitumia lakini hata hivyo baadhi yao bado hawatumii kadi hizo, napenda kusisitiza kuwa ifikapo tarehe mosi mwezi Machi mwaka huu tutasitisha kabisa matumizi ya tiketi za karatasi ili wasafari wote wanaotumia Mabasi ya Mwndokasi watumie kadi" Alisema Dkt.Kihamia

Alisema matumizi ya kadi yanaondoa usumbufu wa kukosekana kwa chenchi lakini pia ni njia muafaka ya kudhibiti uvujaji na upotevu wa mapato ya serikali.

Katika hatua nyingine Dkt.Kihamia alisema Serikali imeshaingia mkataba na mtoa huduma ya Mabasi ambaye atatoa huduma katika awamu ya pili ya mradi wa BRT katika Barabara ya Kilwa kuelekea Mbagala hivyo wananchi wa ukanda ho wakae mkao wa kula.

"Mambo ni mazuri sana Serikali sikivu ya Mh.Dkt.Samia Suluhu Hassan imeshafanya jambo lake kuanzia Machi 31 wakazi wa Mbagala na maeneo ya Jirani wataanza kufaidi huduma ya usafiri wa Mabasi Yaendayo Haraka maarufu kama Mwendokasi jambo ambalo wamelisubiri kwa muda mrefu" Alisema.

Aidha Dkt.Kihamia wakazi wa mbagala nao watatumia kadi janja pale huduma itakapoanza ili kuondoa changamoto za mfumo wa tiketi za karatasi kama zilizojiokeza katika awamu ya kwanza ya mradi.

Awali mwakilishi wa Katibu Mkuu Ofisi ya Rais TAMISEI Mhandisi Gilbert Moga alisema mradi wa TOD japo umekamilika kwa kipindi cha miaka mitatu tangu kuanzishwa kwake Serikali itaona namna ya kuuendelea kwani ni moja ya mambo ambayo yanaleta tija kubwa katika usafiri wa umma hasa kuleta maendeleo kwa wananchi wa pembezoni mwa mradi.

# Bagamoyo inavyozidi kung'arishwa na maendeleo



NA MKWAYU RAMADHANI, BAGAMOYO

VIJIJI na vitongoji kadhaa wilayani Bagamoyo mkoa wa Pwani vili vkuwa giza kutokana na kutopata nishati ya umme, vingine tangu ulipopatikana uhuru wa nchi hii mwaka 1961, lakini sasa maeneo mengi wanatos shukurani kwa Serikali ya Awamu ya Sita kwa kuwezesha kuondoa changamoto hiyo.

Mfano ni Kijiji cha Saadan kilichokuwa katikati ya Hifadhi hiyo ambacho awali iliyogubikwa na giza, umasikini uliochagizwa ukosefu wa huduma za kijamii na kulifanya eneo hilo lisifikike kwa urahisiu kutokea katika miji mikubwa inayolizunguka kama vile yalipo makao makuu ya wilaya, Bagamoyo na Jiji la Dar es salaam.

Nyuma ya miaka ya 1960 hakukuwa na mwanga katika eneo hilo, wenyeji walioshi eneo hilo walijikita katika kazi ya uvuvi wakitumia nyenzo duni, pia kulikuwa na biashara nyingine kama vile ukataji wa ukindu, zao lililotumika sana kwa ajili ya ususi wa mikeka na vikapu, kadhalika ukataji miti ya Mikoko iliyokuwa ikisafirisahwa kwa majahazi kwenda katika miji ya Zanzibar na hata nje ya nchi Mombasa na Visiwa vya Comoro.

Mwanga ulijitokeza mwaka 1962 ilipoanzishwa Bustani ya wanyama, iliyojmumuisha wanyama wachache waliofungiwa katika Ng'enge (Zoo) kubwa na ndogo, zilizoanza kuvuta macho ya watalii kuanza kutembelea kijiji hicho kilichokuwa na wakazi wachache, wengi wao wakitokea maeneo mbalimbali ya nchi na kuafauata biashara ya uvuvi.

Enzi za Ukoloni Saadani iliwahi kukaliwa na Koloni la Waarabu walioendesha biashara ya utumwa, iliyotanabaishwanakuwewpo mabaki ya magofu machache yaliyokuwa yakitumiwa katika biashara hiyo, pia gati kuu la kusafirishia watumwa kutoka bandari ndogo ya Saadani kuelekea Unguja na nchi nyingine za jirani.

Kwa mujibu wa simulizi za wazee wa mji huo hata jina hili la Saadani, lilitokana na Mzee mmoja wa Kiarabu aliyekuwa akimiliki saa ya ukutani, hivyo alipochoshwa na maswali ya kuulizwa muda "Saa ngapi? kila mara akawa anawajibu "kama unataka saa nenda kaangalie ndani.

Kwa vile hakuweza kutamka vizuri maneno ya Kiswahili ndipo alipokuwa akikatisha tu kwa kusema "Saadani" ndipo likazaliwa jina hili.

Ukuaji wa mbuga hiyo ya wanyama iliweza kuupa umaarufu mji huo mdogo ulipo kandoni mwa Bahari ya Hindi kwa kuanza kutembelewa na watalii pamoja na watu maarufu, akiwemo Mwanasiasa aliyeshika nyadhifa mbalimbali serikalini Mzee Rashid Mfaume Kawawa, aliyefika Saadani Mwaka 1974 na kuweka jiwe la Msingi la kumbukumbu ya ujiuo wake na uzinduzi wa bustani hiyo ya wanyama.

Kwa bahati nzuri kijiji cha saadan kiliweza kuonja maendeleo mapema kwa kupata zahanati pamoja na Shule ya Msingi iliyoanza ikiwa na madarasa manne na baadaye ikaendelea na kukamilisha madarasa yote saba, pia kiliwahi kununua gari aina ya Center kwa ajili ya shughuli za kijiji.

Kupitia uwepo wa bustani hiyi ya wanyama kijiji nhicho kilianza kupokea wafanyakazi wengi wakati huo wakijulikana kama 'Game Scout' kutoka maeneo mbali mbali na baadhi waliajiriwa wananchi wakazi wa kijiji hicho na vile vinavyozunguka bustani hiyo kama Uvinje, Buyuni Kuu na Buyuni Kitopeni.

Kwa kuwa mazingira ya hifadhi ya Saadani ni Jangwa wafanyabiashara wenye asili ya India chini ya Kampuni ya Albhai Panju and Sons walianzisha kilimo cha zao la chumvi na kuvuna maelfu ya tani waliyoisafisha kwenda maeneo mbalimbali ya nchi.

Kampunu hiyo iliweka kiwanda chake maeneo ya Malumbi nje kidogo ya Bustani ya Wanyama ya Saadan, na baadaye serikali kupitia Shirika la Madini la Taifa (Stamico) iliweza kuanzisha kiwanda cha kisasa cha uzalishaji chumvi na kupeleka watalaamu wa madini na kuanzisha mradi huo uliokuwa mkubwa sana.

Lakini katika kipindi chote Hifadhi hii iliyopo chini ya TANAPA, iliyoanzishwa mwaka 1962 ikiwa ni pori la akiba na Mwaka 2005, kupandishwa hadhi rasmi na kuwa hifadhi ya taifa, ikashuhudia ongezeko la wahamiaji waliovutwa na upatikanaji wa Samaki aina ya Kamba ambao katika kijiji hicho hujulikana kama Makaji ambayo yalikuwa yakiuzwa kwa bei kubwa na kuwa na maslahi mazuri kwa wavuvi.

Makampuni binafsi kama vile Dar Ocean Product na hata Tafico walikivamia kijiji hicho kwa ajili ya kununua samaki hao kutoka kwa wavuvi wenyewe moja kwa moja.

Lakini katika kipaindi chote hivyo huku zikipita awamu zote tano la utawala wa Serikali ya jamhuri ya Muungano wa Tanzania wana kijiji walikuwa na changamoto mbalimbali za maendelo kama vile ukosefu wa nishati ya umeme na maji.

Kadhalika miundombinu ya barabara inayotokea mwishoni mwa daraja la kisasa la Wami kuingia kulia katika Vijiji vya Mandela na baadaye Miono, Zimbili, Mkange na kuingia Saadan ilikiuwa ipo katika hali mbaya.

Serikali ikaifanyia kazi changamoto hiyo baada ya kufanya ujenzi wa kisasa wa baraba inayotokea eneo la Makurunge Bagamoyo yalipokuwa mashamba ya mifugo ya Ranchi ya Zanzibar Bagamoyo (RAZABA) hadi kuingia Kijiji cha Saadani kupitia miji iliyokuwa kandoni mwa bahari ya Hindi kama vile Mkwaja na Buyuni.

Katika utawala huu wa awamu ya Sita chini ya uongozi wa Rais Dkt Samia Suluhu Hassan, Mbunga ya Saadani inang'aa,baada ya kupatiwa umeme wa kutosha.

Kwa takriban mwaka sasa wakazi wa Saadani wanafaidika na uwepo wa nishati ya umeme, waliyoikosa tangu nchi kupata uhuru.

Kufuatia kupatikana kwa nishati hiyo kijiji cha Saadan kilichokuwa kikikumbana na matukio ya kuvamiwa na wanyama wakati na waharibifu kama vile Tembo na Simba sasa imepungua na kuwa sehemu salama toka kijiji hadi mmbuga yenyewe.

Hivi sasa mkazi wa Saadani atakayetafuta bughudha ya kukutana na wanyama ni yule atayekwenda misituni kwa ajili ya kufanya shuguli za kibinadamu kama vile kuzoa chumvi au kuvua katika maeno yasiyokuwa rasmi kwa shuguli hiyo.

Wakazi wa Saadani kwa sasa wanaliimba jina la Rais Samia kwamba ndiye aliyendika historia ya kuing'arisha Saadani, kizazi kipya kutoka eneo hili sasa hakina tena histoiria ya enzi hizo ambazo wakazi walifuata taa aina ya Karabai iliyokuwa ikiwashwa na wafanyabiasha maarufu enzi hizo Mohamed Mwarabu al maarufu Mzee Ganda na Mfaume Akida Mimi na Sheikh Said waliokuwa wakimiliki maduka zama hizo.



# SERIKALI YAKAGUA UJENZI WA GHALA LA DAWA MSD

NA MWANDISHI WETU

WAZIRI wa Afya Mhe. Jenista Mhagama leo February 6, 2025 ametembelea na kukagua maendeleo ya ujenzi wa mradi wa ghala la Kisasa la kuhifadhia bidhaa za afya linalojengwa na na Bohari ya Dawa (MSD) katika eneo la Kizota, Mkoani Dodoma.

Akizungumza wakati wa ziara hiyo, Mhe. Mhagama amebainisha kuwa serikali ya Rais Samia Suluhu Hassan imefanya mageuzi makubwa katika sekta ya Afya, na imeendelea kujikita kwenye nguzo zinazo tuongozazakimfuno zinazopelekea Ubora wa huduma kwenye sekta ya Afya.

" Kazi zilizofanywa zinaonekana, na hata leo tumeona uwekezaji mkubwa wa ghala la hili kubwa na la Kisasa ambalo lina Ubora wa kimataifa, serikali imewekeza hapa zaidi ya Bilioni 23.7" kujenga ghala hili lenye mita za Mraba 7,200. Alisema Mhagama

Mhe. Mhagama ameongeza kuwa ujenzi huo pia umeendelea kwenye Kanda ya Mtwara, ambapo zaidi ya Bilioni 18 zimetumika kukamilisha ujenzi, huku akibainisha kwamba ujenzi huo pia utaendelea katika Kanda nyingine za MSD ambazo ni Mwanza, Chato, Iringa, Moshi, Arusha na Songea.

"Lengo kubwa la jitihada hizi ni kuhakikisha bidhaa za afya zinapatikana kwa wakati na kwa Ubora unaotakiwa, na zinahifadhiwa katika mazingira yanayotakiwa, hivyo Bodi, menejimenti na Serikali ya Dkt. Samia mmeupiga mwingi. Alisisitiza Mhe. Mhagama.

Katika hatua nyingine Mhe. Mhagama ameupongeza uongozi wa MSD kwa kuboresha upatikanaji wa bidhaa za afya nchini, ambapo amebainisha kwamba hivi sasa upatikanaji huo umepanda hadi kufikia asilimia 83%.

Ameongeza kuwa MSD ni nyenzo muhimu katika uimarishaji wa huduma za afya katika taifa letu.

Mhe. Mhagama ameeleza kuwa Wizara yake itaendelea kushirikiana na MSD Ili kuhakikishandoto na maono haya ya kumkomboa mtanzania, na kuweka usalama kwenye taifa letu yanatimia, kwani afya ya Mtanzania ni usalama wa taifa letu.

# MBARAWA ATAKA KASI UJENZI WA UWANJA WA NDEGE DODOMA

NA MWANDISHI WETU

WAZIRI wa Uchukuzi Prof Makame Mbarawa amehimiza wasimamizi wa ujenzi wa uwanja wa ndege wa kimataifa wa Msalato ambao ni TANROADS na TAA kuhakikisha Mkandarasi anaongeza kasi zaidi ya umaliziaji wa hatua zilizobaki ili kukabiliana na mvua zinazotarajiwa kuanza kunyesha

Mbarawa ameyasema hayo wakati wa ziara yake ya kutembelea na kukagua maendeleo ya ujenzi wa kiwanja kipya cha ndege kilichopo Msalato Jijini Dodoma iliyofanyika Tarehe 30 Januari,2025.

"Ninapongeza kwa dhati hatua zilizofikiwa, nimeona sehemu ya kwanza inayohusisha ujenzi wa uwanja wa kurukia na kutua ndege unaogharimu shilingi Bil 165.65 kazi inaendelea vizuri na imefikia asilimia 84 natoa rai msimamieni Mkandarasi aongeze kasi hapa ili mvua zinazotarajiwa kuanza mwezi Machi mwaka huu zisimkwamishe" amesisitiza Mbarawa.

Amesema Mkandarasi asimamiwe vyema afanye kadri awezavyo na kwa thamani halisi ya fedha uwekaji wa rami umalizike ndani ya wiki mbili sababu mwezi wa tatu kutakuwa na mvua nyingi na huwezi kuweka rami wakati wa mvua.

Aidha ameongeza kuwa kazi zitakazobaki za kufunga mifumo ya kuongozea ndege sambamba na sehemu ya pili ya ujenzi wa jengo la abiria ambao umefikia asilimia 70 ambavyo vinaweza kufanywa taratibu hata kipindi cha mvua vitakamilika mwishoni mwa mwezi Juni, 2025 na uwanja utakuwa tayari kwa matumizi ambapo utaleta tija kwa Nchi na wakazi wa Dodoma na mikoa ya jirani.

Akitoa taarifa za mradi Meneja wa Wakala wa Barabara Mkoa wa Dodoma Mha Zuhura Amani amesema mpaka sasa utekelezaji wa mradi unaendelea vizuri ambapo ujenzi wa uwanja umefikia asilimia 84, na upande wa majengo yote unaohusisha jengo la kushukia na kupandia abiria na jengo la kuongozea ndege vimefikia asilia 51 kwa ujumla na wataongeza kasi ya usimamiaji ili vikamilike kwa wakati na kwa thamani halisi ya fedha ili wananchi waanze kukivunia maendeleo yanayoletwa na serikali ya awamu ya sita inayoongozwa na Rais Dkt Samia Suluhi Hassan.

# Tanzania yapaa sekta ya fedha



NA MWANDISHI WETU

TANZANIA imepiga hatua kubwa kwenye sekta ya fedha kwa mujibu wa ripoti ya Absa ya viashiria vya Masoko ya Fedha - AFMI ( Absa Financial Markets Index ) 2024 iliyozinduliwa leo Jijini Dar es Salaam, ikipanda kutoka alama 50 hadi alama 52, na kujikita katika nafasi ya 12 miongoni mwa mataifa 29 yaliyotathminiwa barani Afrika.

Ikiwa katika mwaka wake wa nane, AFMI ni ripoti maarufu barani Afrika, ambayo hupima maendeleo ya sekta ya fedha katika nchi za Afrika, ikitathmini vigezo sita vikuu, ambavyo ni kuenea kwa soko, upatikanaji wa fedha za kigeni, uwazi kwenye soko na kanuni, maendeleo ya mifuko ya penseni, mazingira ya uchumi ngazi ya kitaifa, na kutekelezeka kwa makubaliano ya kifedha.

Akiongea katika hafla ya uzinduzi wa ripoti ya AFMI , Gavana wa Benki Kuu ya Tanzania, Emmanuel Tutuba, ambaye alikuwa ni mgeni rasmi, alipongeza kundi la makampuni la Absa Group kwa kujitolea kukuza uwazi na ufanisi katika masoko ya fedha barani Africa kupitia ripoti ya AFMI. " Mafanikio yaliyobainishwa katika ripoti hii ni ushahidi wa juhudi za ushirika miongoni mwa serikali, Benki Kuu ya Tanzania, na washirika wa soko la fedha katika kuboresha masoko hayo," alisema.

> **"Pamoja na kuwa kuna maendeleo yamepatikana, bado kuna kazi ya kufanya hasa kwenye maeneo kama mifuko ya pensheni na mifumo wa kisheria,"**

Moja ya maeneo ambayo Tanzania imeonyesha kupiga hatua ni Upatikanaji wa Fedha za Kigeni, ikipanda kutoka alama 53 hadi alama 60, hasa kutokana na Benki Kuu ya Tanzania kuchapisha Miiko ya utendaji katika Soko la Fedha za Kigeni Miongoni mwa Mabenki ( Interbank Foreign Exchange Market code of conduct,), ikiingiza kanuni 52 kati ya 55 zinazotambuliwa kimataifa ( FX Global Code Principles).

Eneo la pili ni Uwazi katika Mazingira ya uchumi ngazi ya Kitaifa, ambapo imepanda kutoka alama 80 hadi 85, ikichagizwa na uwazi, ikiwemo umma kuruhusiwa kufahamu ratiba ya mkutano wa sera ya fedha, mfumuko mdogo wa bei, na kupungua kwa uwiano wa mikopo chefuchefu kwenye makampuni ya biashara.

Eneo la tatu ni uwezo wa soko la fedha kufikia watu wengi zaidi, ambapo maendeleoa katika nyanja hii yanatokana na kutolewa kwa dhamana ya makampuni (corporate bonds) zenye thamani ya Dola za Marekani 300m, na kuziduliwa kwa huduma mbalimbali za kifedha ikiwemo zinazorandana na maadili ya Dini ya Kiislamu.

Naye Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya Absa Tanzania, Obedi Laiser, alisisitiza umuhimu wa ripoti ya AFMI katika kuchochea kukua kwa masoko ya fedha barani Afrika. " Kupanua masoko ya fedha na vilevile kuyafanya yafikie watu wengi zaidi ni muhimu kwa hatua inayofuata ya maendeleo barani Afrika," alisema mkurugenzi huyo. " Tunayo fahari kushirikiana na OMFIF katika kutayarisha ripoti hii, ambayo inafanya kazi kama dira miongoni mwa watunga sera na wawekezaji.

Tukio la uzinduzi wa ripoti ripoti hiyo inayoheshimika ilihudhuriwa na wadau, watunga sera, na watalaam wa masuala fedha, ambapo walipata fursa ya kubadilishana mawazo huku wakitathmini taarifa hiyo na jinsi gani inahusiana na utendaji wa masoko ya fedha nchini Tanzania.

Uzinduzi huo vilevile ulihudhuriwa na maofisa wakuu wa Absa Group, ambao walichangia uzoefu wao kwenye maendeleo yanayojitokeza kwenye sekta ya fedha ambayo yanaamua muundo wa masoko ya fedha Afrika, ikiwemo teknolojia za kidijitali, na juhudi za kuboresha vyombo vya sheria na vinavyosimamia kanuni.

Ripoti hiyo, inayotayarishwa kwa kushirikiana na OMFIF, inatoa taarifa muhimu kwa wawekezaji wa watunga sera, huku ibainisha fursa kwa upande moja, na vilevile maeneo yanayohitaji kufanyiwa maboresho kwenye masoko ya fedha barani Afrika.

Wajkati huohuo, ripoti hiyo imebanisha maneo mawili ambayo Tanzania inapaswa kuyafanyia maboresho, ikiwemo mifuko ya pensheni, ambapo ripoti imedokeza haja ya kuimarishwa kwa uwezo wa kuwekeza wa wadau wa ndani. Na vilevile uboreshaji wa mfumo wa sheria ili kuinua kiwango cha imani ya miongoni wawekezaji.

Richard Magongo, Mkurugenzi wa Bodi - Mwenyekiti wa Kamati ya Ukaguzi na Mazingira Hatarishi, kwa niaba ya Paul Makanza, Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi, Benki ya Absa Tanzania, pamoja na kuwashukuru waliohudhuria hafla hiyo, alisisitiza haja ya kufanyia maboresho ya maeneo nchini Tanzania yalioainishwa kwenye ripoti.

" Pamoja na kuwa kuna maendeleo yamepatikana, bado kuna kazi ya kufanya hasa kwenye maeneo kama mifuko ya pensheni na mifumo wa kisheria," alisema Magongo. " Absa inaahidi kuwa itaendelea kushirikiana na wadau wote kuhakikisha masoko ya fedha nchini Tanzania yanaendelea kukua."

# TAHARIRI

## Usimvunje nguvu mkuu wa nchi anapowaza kutukomboa

KUMEKUWA na maneno ya chini chini kwenye mitandao ya jamii juu ya ziara anazofanya Rais Samia Suluhu Hassan kwenye mataifa mbalimbali duniani.

Ziara ambazo zinasaidia kuifungua nchi kimataifa, kuwapa fursa wawekezaji wa ndani kuona upeo wa dunia lakini pia kuweka mazingira mazuri ya kukaribisha wawekezaji wa nje.

Hata hivyo, wapo wanaoumizwa na ziara hizo. Kwa madai hazina maana, zinatumia fedha za walipa kodi bure bila sababu. Wanakwenda watu wengi kuliko ilivyopaswa kuwa.

Ni kauli za wakosaji, ambazo zimejaa hila, ghiba na choyo kisicho na sababu yoyote. Rais Samia Suluhu Hassan amekifanya kile ambacho viongozi wengi waliopata kukalia kiti chake nchini hawakuweza, au walikifanya kwa udogo.

Kitendo cha kuongozana na wafanyabiashara, wanahabari, wasanii, wanamichezo, wanamazingira na watu wa kada mbalimbali katika ziara zake ni upeo wa juu wa kuwafikiria wananchi wake.

Wanapofika huko watu hao ambao baadhi wanajigharamia nauli na malazi, wanatambulishwa kwa diaspora. Wanatambulishwa kwa wafanyabiashara wakubwa au wasanii wakubwa wa nchi anazotembelea Rais Samia.

Hakuna kitu kizuri kama kupata kiongozi anayefikiria hatma ya wananchi wake, angeweza kwenda mwenyewe kimya kimya kisha akarudi kimya kimya na chochote kisitokee. Lakini ameamua kulifanya hili la kuongozana na watu bado wapo wanaomsakama.

Hatumtendei haki, kwa sababu analifanya hili si kwa kushurutishwa na hakuna namna yoyote iwayo kuwa ananufaika na kitendo hiki zaidi ya kuwa wanaokwenda naye ndio wanaonufaika.

Kama hiyo haitoshi, mbali ya ziara za kitaifa anazofanya anapata wasaa wa kufuatilia mikopo na misaada yenye masharti nafuu kwa ajili ya miradi ya maendeleo ikiwemo hospitali, miundombinu ya barabara, majengo na taasisi za elimu.


## BODI YA UHARIRI

Mhariri Mkuu:
Mhariri Habari za Biashra & Uchumi:

Mhariri wa Habari:
Idara ya Masoko:

## MAWASILIANO

JAMVI MEDIA GROUP





*Sehemu ya watumishi wa Wakala wa Vipimo wakiwa kazini Kituo cha Misugusugu Mkoa wa Pwani.*

# UCHAMBUZI

## Nchimbi -- mshikamano wetu ndio nguzo yetu

ANAANDIKA MSHITITI DK. AHMAD SOVU

KAMA angekuwa mchezaji wa mpira wa miguu wa timu ya Yanga basi Dk. Nchimbi ningemuita Aziz Ki au wa Azam angekuwa Fei toto na kama ni Simba basi ndio Clatous Chama na kama ni Mashujaa basi ndio Reliants Lusajo. Maana amepiga ndipo palipo.

Kupiga huku si kupiga kwa boli hapana, ni kutoa hoja au ukumbusho katika wakati mwafaka na pahala mwafaka.

Akiwa mkoani Singida katika ziara yake ya kwanza kwa mzunguko huu wa pili wa mfululizo wa ziara zake, katibu mkuu wa CCM, Balozi Dk. Emmanuel Nchimbi kwa kinywa kipana kabisa na bila kificho amekemea tabia ya baadhi ya watu wachache kutaka kutugombanisha na kuhubiri chokochoko na kauli za kibaguzi zinazoashiria kuvuruga umoja na mshikamano wetu kama taifa la Tanzania.

Alisema Dk. Nchimbi: "Tusikubali kuacha umoja wetu nawaombeni sana, kama kuna jambo mkienda nyumbani leo na mtu akikuuliza katibu mkuu amesema nini umwambie amesema tusikubali kuacha umoja wetu, tusikubali kugawanywa, tusikubali kufarakanishwa."

Kauli hii ya Dk. Nchimbi imekuja wakati mwafaka kwani ni kweli zipo bishara za baadhi ya watu kuanza maneno yanayoelekea kuuteteresha umoja wetu.

Watanzania ni wamoja na umoja na mshikamano wetu kwa hakika hauna mbadala.

Umoja na mshikamano wetu ndio umetufikisha katika hatua kubwa ya maendeleo iliyopigwa.

Tumeshuhudia mathalan, katika kipindi cha miaka mitatu tu ya Rais Dk. Samia kumepigwa hatua kubwa za maendeleo.

Uendelezaji wa miradi mikubwa ya maendeleo kama vile SGR, umeme katika Bwawa la Mwalimu Nyerere, ujenzi wa miundombinu ya mwendokasi na barabara nchi nzima, ongezeko kubwa la watalii, maboresho makubwa katika sekta ya afya na elimu, maboresho katika sekta ya kilimo, uvuvi, mifugo,michezo, sanaa mawasiliano n.k ni mifano ya umuhimu wa kuwa na umoja, amani na mshikamano kama Taifa.

Hivyo, ni lazima kulinda umoja huu na mshikamano wetu na kuepuka kubaguana kwa misingi ya ukabila, dini, maeneo na matabaka kama alivyosisitiza Dk. Nchimbi kuwa;


"Tanzania lazima iendelee kuwa nchi moja yenye mshikamano, yenye upendo ambayo haibagui watu wake kwa misingi ya ukabila, wala dini wala vyama vya siasa. Wote ni Watanzania, nchi yetu sote tuishi kwa kushirikiana na tupendane."

Kwa hakika, tunatoa kongole sana kwa Balozi Dk. Nchimbi kwa kukumbusha suala hili muhimu na adhimu kwa Taifa.

Tunatoa mwito kwa viongozi wengine wa serikali, dini, vyama vya siasa na vya kijamii na wananchi mmoja mmoja kuendelea kumuunga mkono Dk. Nchimbi kwa kukumbusha na kuonya kwa yeyote atakayeashiria kutaka kuuteteresha umoja wetu.

# UNDP YAJA NA WIKI YA UBUNIFU

NA MWANDISHI WETU




WAKATI Dunia ikienda kasi katika teknolojia Tanzania itanufaika na ushikiano wa Umoja wa Mataifa (UNDP) Tanzania kupitia programu yake ya FUNGUO, Vodacom Tanzania, na Tume ya Sayansi na Teknolojia Tanzania (COSTECH) ambapo ushirikiano huo umefanikisha kuandaa Wiki ya Ubunifu Tanzania 2025 (IWTz2025). Anaripoti Mwandishi Wetu, Dar es Salaam … (endelea).

ushirikiano huu utazidi kuimaisha Tanzania kwenye maendeleo ya Teknolojia na ubunifu. Wiki hiyo itakayoanza tarehe 12 Mei mpaka tarehe 16 Mei 2025 katika kituo cha Mikutano cha Kimataifa cha Julius Nyerere (JNICC), Dar es Salaam. Wakati huo huo kutafanyika mkutano wa Future Ready wa Vodacom.

Kauli mbiu ya mkutano huo itakuwa "Ubunifu kwa Maendeleo Jumuishi na yenye Ustahimilivu", ikilenga kuonyesha dhamira ya pamoja yakujenga jamii endelevu, jumuishi na ya kisasa katika kutatuachangamoto ya ajira kwa vijana kwenye zama hizi za kidijitalina kuchochea ukuaji wa kibiashara kupitia tafiti na ubunifu.

Leo tarehe 5 Februali 2025 Taasisi hizo zimetangaza ushikiano huo mbele ya waandishi wa habari jijini Dar es Salaam.

Mkurugenzi Mtendaji wa Vodacom Tanzania, Phillip Besiimire amesema ushirikiano huo utaleta mabadiliko katika sekta ya ubunifu nchini Tanzania, kwa kuunganisha wabunifu na wajasiriamali wa kimataifa kutoka sehemu mbalimbali za dunia.

"Tunalenga kuleta mitazamo na taaluma za kimataifa kwenye mijadalahii na kuifanya Tanzania kuwa kitovu cha mabadiliko yakidijitali, sambamba na kuanzisha mifumo ya ikolojia yaubunifu inayoongozwa na vijana.

"Jitihada za Vodacom za kutumia teknolojia kwa lengo la kuboresha maisha ndiozinazounda msingi wa ushirikiano huu unaoendeshwa na maonoyanayofanana ya kuwawezesha watanzania kuendelea kupitiaUchumi wa kidijitali ulioendelevu na jumuishi."

Aidha amesema kuwa mkutano wa Vodacom wa Future Ready Summit (FRS2025) ni tukio linaloweka msingi wa maadhimisho hayo pamoja nakuibeba kauli mbiu ya "Kubadilisha hatma ya miji: Usasa, Uendelevu na Jumuishi", ambayo inazungumzia umuhimu wa kuibadili miji ya Tanzania kwa ajili ya kutatua changamoto zinazotokana ukuaji wa kasi, mabadiliko ya tabia nchi namabadiliko ya teknolojia.

Kwa upande wake Mwakilishi Mkazi wa UNDP Tanzania, Shigeki Komatsubara, amesisitiza dhamira ya UNDP ya kujenga mfumo wa ubunifuulio jumuishi na wenye ustahimilivu.

"Tunatambua kuwa ubunifu ni nyenzo muhimu katika kushughulikia changamoto za maendeleo endelevu na kuunda fursa shirikishi. Kupitiaushirikiano huu, tunalenga kuwainua Watanzania, hasa vijana nawanawake, kuwa chachu ya mabadiliko chanya.

"Wiki ya Ubunifu Tanzania 2025 (IWTz2025) itaonyesha ari ya ubunifuTanzania kwenye jukwaa la kimataifa, kuvutia uhamasishaji naushirikiano kupitia na mifumo iliyofanikiwa duniani."

Kuhusu ajenda zitakazohusika katika maadhimisho ya Wiki ya Ubunifu ni hayo itahusisha mijadala mtambuka, warsha na maonyesho, huku lengo likiwa ni Mustakabali wa miji mahiri, endelevu na jumuishi, Uwezeshaji wa vijana kwenye zama za kidijitali, Uboreshaji wa tafiti na ubunifu kwa ajili ya biashara

Akizungumza kwa niaba ya Serikali, Mkurugenzi wa Kituo cha Maendeleo na Uhamisho wa Teknolojia kutoka Tume ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH), Dk Athumani Ngumia alisema mchango muhimu wa ushirikiano huo ni kukuza ubunifu.

"COSTECH imejidhatiti kuwaunganisha wadau kwa lengo la kuchochea utafiti, teknolojia na ubunifu ambao unaendana navipaumbele vya nchi katika maendeleo na maono ya mwaka2050. Maadhimisho ya Wiki ya Ubunifu kwa mwaka 2025 nijukwaa pekee kwa ajili ya sekta binafsi na umma kupeleleza nakutekeleza masuluhisho kwa ajili ya ukuaji endelevu."

Wiki ya ubunifu 2025 (IWTZ2025) na mkutano wa Future Ready Summit (FRS2025) inatarajia kuwaleta pamoja washiriki, wazungumzaji na wabunifu kutoka Tanzania, Afrika na sehemu mbalimbali duniani na kuwa jukwaa muhimu la kubadilishana maarifa, kuendeleza ushirikiano wenye tija na kuhamasishamawazo yenye kuleta mabadiliko.

Washiriki wa matukio haya wanahamasishwa kutekeleza shughuli mbalimbali sambamba na matukio hayo muhimu kwa lengo la kuhakikisha watu wengi zaidi nchini wanawezakunufaika na mikutano hiyo itakayo kuwa inafanyika kwenyeKituo cha Kimataifa cha Mikutano cha Julius Nyerere.

Wakati huo huo Meneja Program kutoka FUNGUO Joseph Manirakiza ametumia nafasi hiyo kuelezea kwa kina umuhimu wa ushirikiano huo sambamba na kutambua mchango wa bunifu katika kukuza maendeleo endelevu

Kuhusu Programu ya FUNGUO ni kwamba inajitolea kuendeleza Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDGs) nchini Tanzania kwa kutumia mbinu shirikishi inayolenga kusaidia maendeleo ya biashara bunifu na zinazozingatia athari chanya kwa jamii, hususan kwakuimarisha mazingira ya ubunifu kwa wajasiriamali na biasharandogo na za kati (MSMEs).

Aidha FUNGUO inatambua kuwa kusaidiana kukuza biashara hizo siyo tu kutachangia kuongeza ajira, hususan kwa wanawake na vijana, bali pia kutaboresha kipato, kuboresha hali ya maisha, na kuchochea maendeleo jumuishi naendelevu.

Pia Mpango huo unafadhiliwa kwa pamoja na Umoja wa Ulaya(kupitia Mpango wa BEGIN), Serikali ya Uingereza (kupitiaMpango wa Ushirikiano wa Teknolojia na Ubunifu barani Afrika – ATIP), na Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa(UNDP).

FUNGUO unatekelezwa na UNDP Tanzania kwa kushirikiana na Mfuko wa Maendeleo ya Mitaji wa Umoja waMataifa (UNCDF). Ushirikiano huu wa wadau mbalimbali unahakikisha ufanisi na athari chanya katika mazingira yaubunifu nchini Tanzania.

Kwa kushirikiana kwa karibu na Tume ya Sayansi na Teknolojia Tanzania (COSTECH) pamoja nataasisi nyingine za serikali, FUNGUO inalenga kuchangia maendeleo endelevu nchini kwa kuweka mazingira wezeshi kwabiashara bunifu na MSMEs.

Kuhusu Vodacom Tanzania ni mtoa huduma wa mawasiliano anaeongoza nchini Tanzania, ikiwa na mtandao wa data wa kasi zaidi. Tunahudumia zaidi ya wateja milioni 26.3. Vodacom Tanzania na kampuni zake tanzu ni sehemu ya Vodacom Group yenye usajili nchini Afrika Kusini, ambayo nayo inamilikiwa naVodacom Group Plc yenye makao makuu Uingereza.

Wakati COSTECH ni Tume ya Sayansi na Teknolojia Tanzania iliyoanzishwa kupitia Sheria ya Bunge Na. 7 ya mwaka 1986.Pia ni shirika la umma linalohusika na kuratibu na kukuza shughuli za utafiti na maendeleo yateknolojia nchini.

Pia, inatoa ushauri kwa serikali kuhusumasuala yote yanayohusiana na sayansi, teknolojia, na ubunifu(STI) kwa lengo la kuchangia maendeleo ya kiuchumi na kijamiinchini Tanzania.COSTECH inafanya kazi chini ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia.

*Picha mbali mbali za Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk. Philip Mpango na Mwenza wake Mama Mbonimpaye Mpango, pamoja na viongozi wengine wa serikali wakiwa katika msiba wa marehemu Sekunda Massawe ambaye ni Mama mzazi wa Waziri wa Elimu Sayansi na Teknolojia, Profesa Adolf Mkenda baada ya Ibada iliyofanyika katika Kanisa Katoliki Parokia ya Mtakatifu Pius X - Tarakea mkoani Kilimanjaro, jana.*










*Picha mbali mbali za Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk. Philip Mpango na Mwenza wake Mama Mbonimpaye Mpango, pamoja na viongozi wengine wa serikali wakiwa katika msiba wa marehemu Sekunda Massawe ambaye ni Mama mzazi wa Waziri wa Elimu Sayansi na Teknolojia, Profesa Adolf Mkenda baada ya Ibada iliyofanyika katika Kanisa Katoliki Parokia ya Mtakatifu Pius X - Tarakea mkoani Kilimanjaro, jana.*

# SIMU YAKO INAVYOWEZA KUBAINI TATIZO LA MOYO



NA MWANDISHI WETU

MATATIZO ya kuganda kwa damu ni makubwa, Ikiwa damu yako itaganda kwa kiasi cha chini, uko katika hatari ya kuvuja damu, jambo ambalo linaweza kukusababishia kutokwa na damu hadi kufa. Ikiwa damu yako itaganda kabisa , uko katika hatari ya hali iitwayo 'thrombosis', ambayo inaweza kusababisha mshutuko wa moyo.

Madaktari wanaweza kupima kuganda kwa damu lakini wanahitaji sindano iliyojaa damu yako kabla ya kufanya hivyo. Lakini hivi karibuni unaweza kuwa na uwezo wa kufanya vipimo mwenyewe nyumbani kwa kutumia rununu yako.

Mapema wiki hii Martin Cooper, mwanamume aliyeongoza timu iliyotengeneza simu ya rununu ya kwanza kabisa - alitabiri kwamba anaamini kuwa simu za rununu zitakuwa chombo muhimu cha kufuatilia afya zetu . Ahadi hiyo tayari inatimizwa.

Mnamo Machi 2022, wanasayansi katika Chuo Kikuu cha Washington walitumia iPhone kugundua kuganda kwa tone moja la damu. Walitumia kihisi cha kifaa cha Lidar (kinachotambua mwanga ), ambacho hutumia miale inayopigika kuunda picha za 3D za mazingira ya simu.

> *Kifaa hicho kinaweza kuwa njia "ya bei nafuu, rahisi na nzuri" ya kutambua wagonjwa wanaohitaji uchunguzi zaidi, wanasema madaktari wa magonjwa ya moyo katika Kituo cha Kitaifa cha Magonjwa ya Moyo na Mishipa nchini China, ambao walihusika na utafiti huo.*

Ni teknolojia inayoruhusu kifaa chako kuchukua vipimo sahihi vya vitu au umbali ili kuchanganya ulimwengu halisi na pepe na uhalisia ulioboreshwa. Kwa mfano, inaweza kuonyesha jinsi fanicha inavyoweza kuonekana katika chumba chako na pia inaweza kusaidia kuboresha umakinifu wa kiotomatiki unapopiga picha.

Lakini inageuka kuwa sensa ni sahihi kutosha kuchukua mgando katika damu - na mgando wa maziwa.

Mipigo ya leza hutoa "mifumo ya doa" tofauti kwani mwanga hutawanywa na kioevu, kulingana na mnato wake. Kutenganisha kiwango cha mafuta katika maziwa, kwa mfano, hubadilisha muundo kwa njia inayotambulika, kama vile damu inavyoganda.

Watafiti waligundua waliweza kutofautisha kati ya damu iliyoganda na ile ambayo haijaganda kutoka kwa tone dogo lililowekwa kwenye slaidi ya glasi. Katika hatua za hivi majuzi zaidi, timu pia ilitumia gari na kamera kwenye simuya rununu kufuatilia msogeo wa chembe ya shaba kwenye tone la damu ili kutathmini mgando.

thChanzo cha picha,Getty Images

Watafiti wengine wamekuwa wakibuni mbinu zinazotumia kamera katika simu yako kupima vipengele vingine vya afya ya moyo, kama vile shinikizo la damu.

Watafiti katika Chuo Kikuu cha Toronto, Canada, na Chuo Kikuu cha Hangzhou, huko Zhejiang, Uchina, wamebuni kanuni za algoriti ambazo zinaweza kuchukua mabadiliko yasiyoonekana katika mtiririko wa damu usoni kutokana na video zilizojipiga kwa kutumia kamera zinazotazama mbele kwenye simu za rununu .

Timu nyingine ya wanasayansi wa Kichina imeunda algorithms ya kujifunza kwa kina ambayo inaweza kuchukua alama zingine za afya ya moyo kutoka kwa picha nne zilizopigwa kwa kutumia simu ya rununu - mtazamo wa mbele, na moja ikitazama chini kutoka juu ya kichwa. Algorithm ilionekana kuzingatia mabadiliko ya hila katika mashavu, paji la uso na pua hasa , kama vile mikunjo ya uso na amana ya mafuta chini ya ngozi ambayo ni vigumu kuchunguza kwa jicho la mwanadamu.

Inaweza kutambua kwa usahihi ugonjwa wa moyo katika 80% ya visa, ingawa haikubainisha hatari katika 46% ya kesi, maana inaweza kusababisha wasiwasi usio wa lazima kati ya wagonjwa ikiwa hawatatafuta uchunguzi wa kitaalamu zaidi wa matibabu.

Kifaa hicho kinaweza kuwa njia "ya bei nafuu, rahisi na nzuri" ya kutambua wagonjwa wanaohitaji uchunguzi zaidi, wanasema madaktari wa magonjwa ya moyo katika Kituo cha Kitaifa cha Magonjwa ya Moyo na Mishipa nchini China, ambao walihusika na utafiti huo.

Pia kuna matumaini kwamba simu za rununu zinaweza kutoa njia ya bei nafuu na rahisi zaidi ya kugundua magonjwa ya moyo kwa bidii zaidi.

Jennifer Miller, daktari bingwa wa magonjwa ya moyo katika Hospitali ya Watoto ya Los Angeles, na wahandisi katika Chuo Kikuu cha Kusini mwa California, wametengeneza kichanganuzi cha simu cha mkononi kinachoweza kuunganishwa na simu mahiri ili kutoa picha za kitaalam za ndani ya kifua - 'echocardiograms' zinazoweza kufuatilia jinsi damu inavyotiririka kwenye moyo .

Ingawa nyingi za teknolojia hizi bado ziko katika hatua za utafiti na majaribio ya ukuzaji, kuna baadhi ya njia za kuangalia afya yako ukitumia simu yako .

# Nasubiri kuona ubavu wa Tundu Lissu

NA MWANDISHI WETU
MZEE MZIMA STEVEN WASSIRA

TUSIPOUSEMA ukweli adui zetu watausema. Tusisubiri adui watusemee." Hiyo ilikuwa kauli ya mwisho ya Samora Moises Machel, Rais wa kwanza wa Msumbiji alipowahutubia wajumbe kama Mwenyekiti wa FRELIMO. Hakusema nao tena kwani alifariki kwenye ajali ya Ndege.

1. Kalamu yangu itasema nanyi watatu, Steven Wassira, Emmanuel Nchimbi na Tundu Lissu, sitachoka kwasababu hatima ya Watanganyika iko mikononi mwenu, mnaweza kuitengeneza ama kuimwaga.

2. Yale ambayo wajumbe wa kamati kuu na Halmashauri kuu zenu hawatayasema, kalamu yangu itasema nanyi bila kupunguza wala kuzidisha.

3. Wataalamu wetu wakiwanyamazia ili kulinda ulaji wao, kalamu yangu itasema nanyi bila kumung'unya maneno.

4. Naanza na CCM ambayo wajumbe walikutana kumpitisha (kumthibitisha) Makamu Mwenyekiti wao Steven Wasira, wakampitisha pia mgombea wa Urais, Mama Samia Suluhu Hassan na mgombea mwenza wake, Dkt Emmanuel Nchimbi. Walifanya hivyo kwasababu wanaweza na hakuna wa kuwapinga.

5. Lakini leo nawakumbusha hotuba ya Nyerere, aliyoitoa tarehe 05. Februari, 1978 wakati CCM ikiadhimisha mwaka mmoja wa kuzaliwa kwake na miaka 11 tangu kutangazwa kwa Azimio la Arusha.

6. Kwenye uwanja wa Jamhuri mjini Dodoma, Rais Nyerere kama Mwenyekiti wa chama tawala CCM, alihutubia kwa maneno makali, yaliyoonyesha hasira na hisia kali, aliwafananisha wala rushwa na malaya, akasema "tunafuga malaya ndani ya Ofisi."

7. Nyerere kuonyesha alivyoichukia rushwa, alitoa mwito chama kisafishwe na kwamba huko serikalini atapambana na wala rushwa vilivyo, akahamisha na kukitoa Kikosi cha kuzuia Rushwa, kwenye Ofisi ya Waziri Mkuu, akakiweka kwenye Ofisi ya Rais, ili kifanye kazi chini ya maelekezo yake.

8. Nyerere aliashiria wazi hakuwa na simile na "mlarushwa."

9. JE, CCM ya leo inawafananisha wala rushwa na nani?

10. Chama chochote kilichoachia rushwa kutamalaki hadi kugeuka utamaduni unaotawala watu kwenye maisha ya siku kwa siku, hakiwezi kuunda serikali nzuri. Lazima kitaunda serikali mabaya kuanzia ngazi ya chini hadi serikali kuu.

11. Mambo haya Ufisadi, upiga dili, ubadhirifu wa fedha za serikali, uzembe wa kutokuwajibika, yanapotawala, lazima wananchi watakuwa na kilio kisichokoma.

12. Hapa ndipo wanaoongoza vyama wanapaswa kuelewa, kwamba serikali inayowatawala wananchi inaundwa na chama kinachoshinda kwenye uchaguzi. Kwahiyo uchaguzi wowote usiokuwa wa haki, hautawawezesha wananchi kuwata viongozi wazuri, mfumo mbaya utawachekecha wazuri, utawatupa kando na kuwasimika viongozi wabaya, ambao wataendeleza utawala mbaya.

13. Mzee Wasira, unapoiandaa CCM kushiriki kwenye uchaguzi mkuu ujao, uweke akiba moyoni mwako, kwamba uchaguzi wa 2024 umewaacha wengi wakiwa majeruhi, kuanzia wagombea, wapiga kura hadi wananchi wanaotawaliwa.

14. Inakupasa uelewe unakwenda vipi na hao majeruhi? Unachukuliana vipi na umma uliojeruhiwa? Ushindi wa hao walioshinda unatafsirika kwenye maisha ya siku kwa siku ya mwananchi! JE, ushindi wa mpiga kura utaonekana wapi? JE, utaonekana kwenye wingi wa kura zilizohesabiwa?.

Ushindi wa mgombea unaotangazwa na msimamizi, naam unaosherehekewa na mgombea aliyeshinda na hao wanaomshabikia, inabidi ugeuzwe kuwa ushindi wa mpiga kura kwa kuonyesha matunda kwenye maisha ya siku kwa siku ya wananchi chini ya kiongozi huyo.

15. Hapa namaanisha uwajibikaji kupitia uongozi mzuri na utawala bora.

16. Mgombea aliyeshinda kwa mizengwe anapotawala ama kuongoza vizuri, huwasahaulisha maumivu yao, hao walioshindwa. Lakini balaa hugeuka janga hapo uchaguzi unapoendeshwa isivyo haki, ukatoa uongozi na utawala usiojali haki! Hapo wanaotawaliwa huwa wamewekwa kwenye maumivu yasiyokoma.

17. Hiyo hali ngumu ndiyo huwasukuma kuhoji uko wapi ushindi wa mpiga kura?

18. Mitaani, vijijini na vitongojini, wapo walioshinda lakini hawawezi kuitisha hata mkutano wa hadhara wananchi wakawasikiliza! Wapo wanaotembea na mihuri mfukoni wakisubiri wateja, yaani wananchi wanaokuja wakihitaji barua ama kujaziwa fomu.

19. Huo ulaji rushwa ulioko ngazi za chini, ninyi mlio juu mnapaswa kuushughulikia kwa ukali unaoonekana wazi wazi, hili mlifanye kabla ya uchaguzi mkuu, kwani wananchi siyo misukule, wanajua jema la kuchagua na baya linalopaswa kulinyimwa kura.

20. Wakubwa wa vijijini na vitongojini wana madaraka kuliko Rais Samia, maana mkubwa akiwaambia mgambo "huyo mwekeni ndani" kauli yake inatosha kumsotesha raia mwema wiki mbili hadi tatu kwenye rumande zao watawala, hadi atakapounua uhuru wake. Wapo waliojijengea mazingira ya kuogopwa, hawatofautiani na makamanda wa NAZI ya Adolf Hitler. Kumbukeni huyo Hitler aliingia madarakani kidemokrasia, lakini akaishia kutawala kifashisti.

21. Ninyi mnapaswa kusawazisha mambo kabla hasira ya umma haijapata pa kutokezea, maana ikijitokeza haitadhibitiwa wala hakuna awezaye kutabiri yatakayotokea.

22. Kuna suala la Zanzibar kuuasi Muungano! Wazanzibari wanaonyesha uhuru unaoonyesha wazi Rais Samia hana mamlaka dhidi yao.

Hilo Watanganyika wanaliangalia tu, hata kama hawalisemi. Lakini kimya chao Watanganyika siyo ndio mwisho wala siyo suluhisho, hali hii haitabiriki.

23. Tundu Lissu umerithi CHADEMA iliyojeruhiwa, iliyodhoofishwa na kuvurugwa! CHADEMA isiyokuwa na "structure" yenye uongozi wa kitaifa tu, ikiwa haina mizizi kwa wananchi waishio vijijini na vitongojini. Hili kisiasa lihesabuni sawa na dhambi.

24. Kwasababu CHADEMA ina umri wa miaka 33, mmepokea ruzuku tangu 1995 hadi sasa, mlipaswa kuwa na ofisi zenye hadhi kila mkoa, kila wilaya na kwenye majimbo yote nchini. Lakini mwaka 2024 CHADEMA iliweka wagombea 10,000 tu, wakati nafasi zilizogombewa ni 164,000.

Huu ni udhaifu mkubwa, inamaanisha kwenye vijiji na vitongoji 150,000 CHADEMA haina wawakilishi.25. Msidanganyike kwamba mtavuna kura za wananchi kutokana tu na umaarufu mliojitengenezea kupitia vyombo vya habari. Katika nchi hii kura mtazipata kupitia wawakilishi wenu na si vinginevyo.



# USAID YAJIONDOA MITANDAONI GHAFLA

NA MWANDISHI WETU



WAKATI joto likiendelea kupanda la kusitishwa kwa miradi ya afya, Shirika la Misaada ya Kimataifa (USAID), limejiondoa kwenye mitandao ya kijamii na kufunga tovuti yake, huku wafuasi wa Chama cha Demokratiki wakifanya maandamano na kupinga uamuzi wa Rais wa Marekani, Donald Trump kusimamisha shughuli zake kwa siku 90.

Aidha, kumekuwa na maoni tofauti kuhusu uamuzi huo, baada ya Mbunge wa Jimbo la Nzega Vijijini, Dk. Hamis Kigwangala, akipendekeza nchi za Afrika kuwekeza zaidi katika sekta ya afya ili kuwahakikishia wananchi wake wote huduma bora na sio kutegemea wafadhili.

Nipashe ilitembelea akaunti mbalimbali za USAID na kubaini kutokuwapo hewani tangu Februari 4, mwaka huu tovuti na kurasa za mitandao ya kijamii hazikuwa na maudhui yoyote na jana tovuti ilikuwa na taarifa kuhusu mpango wa kuwapumzisha wafanyakazi wake.

Kupitia ukurasa wake wa X, Dk. Kigwangala alisema muda wa kutegemea wafadhili umepita na kwamba ni lazima nchi hizo zibuni mbinu mpya na za kisasa za kugharamia afya za watu wake.

Alisema, kupungua kwa fedha za wafadhili katika sekta ya afya barani Afrika ni changamoto kubwa inayohitaji hatua za dharura kutoka kwa serikali za bara hilo.

"Muda wa kutegemea wafadhili umepita. Ni lazima tubuni mbinu mpya na za kisasa za kugharamia afya za watu wetu," alisema Dk. Kigwangala.




Alisema ni muhimu kuwa na mkakati madhubuti kama wa bima ya afya kwa wote, kodi maalum za kulipia bima kwa watu wasio na uwezo pamoja na kuhakikisha kila mtu anakuwa na bima ya afya.

Dk. Kigwangala ambaye ni mtaalamu wa afya ya jamii mwenye Shahada ya udaktari wa binadamu na Shahada ya Uzamili ya afya ya jamii (MPH), alishauri kuwa na utaratibu mzuri wa matumizi ya rasilimali kwa uwazi, ubunifu na uwajibikaji ili kuboresha mfumo wa afya na kupunguza utegemezi wa misaada ya nje.

Kupitia akaunti zake hizo za kijamii, Dk. Kigwangala alipendekeza mbinu za kisasa za kugharimia afya za watu ikiwa ni pamoja kila Mtanzania kuwa na bima ya afya.

"Kwa Tanzania watu wasio na uwezo ni asilimia 26.4 sawa na watu milioni 16.3, kama hao watahitaji kuchangiwa na serikali, fedha Sh. trilioni 2.445 sawa na Sh.150,000 kwa kila mtu.

"Sheria ya bima ya afya kwa wote namba 13 ya mwaka 2023, kwenye

Inaendelea Uk. 13

# USAID YAJIONDOA MITANDAONI GHAFLA

Inatoka Uk. 12

kifungu cha tano, tayari inalazimisha kila Mtanzania kuwa na bima ya afya, bila kujumuisha watu wengi, mfumo unaweza kuwa dhaifu kifedha na kushindwa kufanikisha huduma bora kwa wote," alisema Dk. Kigwangala.

Alipendekeza kwamba bima ni lazima itoe huduma muhimu za afya ikiwa ni pamoja na kinga, matibabu na huduma za dharura, ambazo zinapaswa kuwa za ubora wa juu.

Alisema mfumo wa bima ya afya Tanzania, unapaswa kulinda watu dhidi ya mzigo wa gharama kubwa za matibabu na kwamba chanzo cha fedha kinapaswa kuwa endelevu katika tozo za bima, michango ya serikali na vyanzo vingine vya fedha.

Alipendekeza kwamba, mfumo wa utozaji wa tozo unapaswa kuwa wa haki, wenye kipato kikubwa wanachangia zaidi ili kusaidia makundi yenye kipato cha chini.

Kadhalika, alipendekeza kanuni za bima ya afya kwa wote za mwaka 2024 zirekebishwe ili kuweka wazi vyanzo vya fedha kwa ajili ya watu wasio na uwezo, namna ya kuwatambua wasio na uwezo na namna ya kuusimamia mfuko wa watu wa kundi hilo.

Dk. Kigwangala ametoa mapendekezo hayo kutokana na agizo la Rais wa Marekani Donald Trump la kusitisha misaada ya usambazaji wa dawa za Virusi vya Ukimwi, Kifua Kikuu na Malaria (PEPFAR) na miradi mingine.

Taarifa iliyotolewa na USAID ilieleza kuwa kuanzia Ijumaa saa 11: 59 jioni, wafanyakazi wote wa USAID walioajiriwa moja kwa moja duniani watapewa likizo ya usimamizi, na kwamba wafanyakazi waliotenguliwa kushughulikia majukumu muhimu ya shirika, uongozi mkuu, na programu maalum wataendelea na kazi kama kawaida.

Ilieleza kuwa wafanyakazi walioteuliwa kuendelea na kazi watapewa taarifa rasmi kutoka kwa uongozi wa Shirika, Februari 6, mwaka huu saa 3:00 usiku.

Aidha, wafanyakazi walio nje ya Marekani, Shirika kwa kushirikiana na Idara ya Mambo ya Nje ya Marekani, inajipanga kuwarejesha nchini humo ndani ya siku 30, kulingana na taratibu za sheria husika.

USAID imetangaza kusitisha baadhi ya mikataba ya Huduma za Kibinafsi (PSCs) na Mikataba ya Huduma ya Ushirika (ISCs) ambayo haijatajwa kuwa ya msingi.




Jana wabunge Democratic nchini Marekani wameandamana wakisema uamuzi huo ni kinyume na uamuzi wa kumteua Mfanyabiashara Elon Musk kuwa Mkuu wa Kitengo cha Ufanisi wa Serikali si sawa kwa kuwa hana mamlaka ya kufungwa kwa shirika hilo.

Mbunge Gerry Connolly akizungumza kwenye maandamano hayo, alisema hakuna mtu yeyote anayeweza kuvunja shirika hilo, bali ni Bunge pekee lenye nguvu hiyo.

Hata hivyo, Trump amemtetea Musk kuwa hawezi kufanya chochote bila idhini ya Ikulu na hatua ya kuvunjwa kwa shirika hilo amepewa baraka na serikali.

Waziri wa Fedha, Mhe. Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba (Mb), akieleza utayari wa Serikali wa kutoa fedha kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya kimkakati ya sekta ya elimu na afya ikiwemo kukamilisha kwa maboma yaliyojengwa na wananchi, bungeni jijini Dodoma. (Picha na Kitengo cha Mawasiliano Serikalini, Wizara ya Fedha).



# AFCON YAZIDI KUPAMBA MOTO




>> Inatoka uk. 16

CHAN na AFCON.

Ameyasema hayo hivi karibuni alikuwa akishiriki Tamasha la Michezo la Bunge Bonanza lililofanyika kwenye Viwanja vya Shule ya Sekondari ya John Merlin jijini Dodoma.

Amesema kuwa tayari ukaguzi wa baadhi ya viwanja umefanyika na vimeonekana kukidhi vigezo "Viwanja vilivyokaguliwa vipo Tanzania bara na Visiwani, na kazi bado inaendelea, lengo ni kuhakikisha michuano hii inafanyika kwa ufanisi"

Mheshimiwa Majaliwa amesema ni vyema sasa Watanzania wakajipanga kutumia fursa zitakazo jitokeza kutokana na kuwepo kwa michuano hiyo hapa Nchini. "Hii ni fursa kwetu Watanzania, lazima tujipange kutumia fursa za kiuchumi zitakazojitokeza, ili tuweze kunufaika".


Aidha, Mheshimiwa Waziri Mkuu amempongeza Spika wa Bunge Dkt. Tulia Ackson kwa kuandaa Tamasha la Michezo la Bunge Bonanza ambalo limewakutanisha wabunge na wanamichezo mbalimbali wa Mkoani Dodoma.

## RASHFORD ATUA ASTONVILA

BARCELONA, HISPANIA

WAWAKILISHI wa mshambuliaji wa Manchester United, Marcus Rashford wamekutana na viongozi wa Antonvila siku ya Jumanne huku mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 27 akitafuta njia ya kuondoka ndani ya kikosi hicho.

Rashford kumekuwa na uvumi wa kutakiwa na timu kadhaa, hivyo kuzidi kufanya uvumi wa kuondoka kwake kushika kasi zaidi, huku hayo yakija wakati Paul Scholes akisema, ndani ya kikosi hicho kuna wachezaji wanane wabovu.



## LUIZ ANAKWENDA HAPA

MILAN, IITALIA

TIMU ya Juventus wameipa Chelsea fursa ya kumsajili kiungo wa kati wa Brazil Douglas Luiz, 26, ambaye pia ananyatiwa na Manchester City na Arsenal.

Hayo yaja huku kiungo wa Ufaransa Paul Pogba, 31, anazingatia ofa kadhaa kutoka kwa timu za ligi tano kuu za Ulaya, lakini makubaliano ya mkataba hayajafikiwa.



# P-SQUARE 'Mapacha' ndani ya mgogoro!-4

LOGOS, NIGERIA

Ni lazima nieleweke kwamba mashabiki hawakupenda P-Square kwa sababu ya nani aliimba au kucheza zaidi. Kilichotufanya tufanikiwe ni ubora wetu hali yetu iliotokana na juhudi zetu za pamoja – sisi wawili! P-Square ilikuwa ya nguvu, na mashabiki waliipenda P-Square kwa sababu ya upekee wetu na umoja, "aliongeza.

Pia alimkosoa Paul kwa kujilinganisha na Jude, akisema kuwa mienendo ya familia ilikuwa na jukumu kubwa katika matatizo ya bendi. "Ulimvunjia heshima mke wangu, familia yangu, kipaji changu, mawazo yangu na hata kuchukua upande wa Jude wakati alipokuwa anajaribu kunikandamiza."

Katika kukamilisha ujumbe wake, Peter alielezea kusikitishwa kwake na hali ya sasa na athari ambayo P- Square imekuwa nayo kwa mashabiki wao. "Sasa nahisi kama umechukua mambo hata zaidi kwa kujaribu kuwageuza mashabiki dhidi yangu kwa kuwafanya wafikiri nina wivu kwako. Umefanya kila kitu unachoweza kuwafanya mashabiki wanichukie, lakini unajua nini? Hawatanichukia kamwe; badala yake, watatuchukia sisi sote kwa sababu tuliwavunja moyo na kuwaangusha."

# DRAKE AFICHUA SIRI YA MAFANIKO YAKE



LOS ANGELES, MAREKANI

SUPASTAA wa muziki wa Hip hop, Drake, amesema siri ya mafanikio yake ni kujifunza kutoka kwa waliofanikiwa.

Drake mwenye umri wa miaka 38, amesema tangu alipokuwa mdogo, alipenda kufuatilia maisha ya mastaa na kuvutiwa na hatua zao kwenye maisha.

Mshikaji huyo mzaliwa wa Toronto, alianza rasmi safari yake ya muziki mwaka 2006 kupitia 'mixtape' yake ya 'Room for Improvement.'

# Tamasha la muziki 'Kadanse ya Mama' yakumbusha enzi za Gurumo na Bitchuka

NA MWANDISHI WETU

TAMASHA la Muziki wa dansi lililoitwa Kadanse ya Mama lilifanyika juzi Jumamosi katika Viwanja vya Ledrs Kinondoni Jijini Dar es Salaam na kushudiwa na umati wa mashabiki huku bendi zaidi ya kumi zikitumbuiza.

Miungoni mwao ni bendi kongwe Msondo Ngoma Music Band iliyoazishwa tangu mwaka 1964 pamona na Mlimani Park iliyozaliwa mwaka 1978, bendi hizi zilipitiwa na wanamuzki mbalimbali wakiwemo maarufu Muhidin Maalim Gurumo ambaye ameshatangulia mbele ya haki na Hassan Rehani Bitchuka ambaye kwa sasa amepumzika masuala ya muziki.

Wanamuziki hao wanakumbukwa kutokana na kila bendi kati ya hizo mbili kuwa na wanamuziki wanaonakiri sauti zao na hivyo kusikika kama wakongwe hao walikupo jukwaani.

Ttukiacha historia ndefu ya jinsi waimbaji wawili nguli Muhidin Gurumo na Hassan Bitchuka walivyokutana kwa mara ya kwanza mwaka 1973 katika bendi ya NUTA Jazz, baadaye wakakutana tena katika miaka na bendi tofauti, lakini mkutano wao wa mwaka 1991 ulikuwa na kishindo kikubwa.

Mwaka huu miamba hii ilikutana tena katika bendi ya Juwata Jazz, hii ni baada ya misele ya kuingia na kutoka mfano kwenda Mlimani park na kisha Orchestra Safari Sound, hapa walikutana tena.


Tena basi katika mkutano huo mabingwwa hawa wa uimbaji hawakuwa hao wawili tu, bali waliwakuta wenzao waliokwisha jijingea mahaba makubwa kwa mashabiki kutokana na uwezo wao wa kuimba na pia tungo zao bora.

Katika safu ya uimbaji pia alikuwepo TX Moshi William, Joseph Maina, Juma Akida, Isaya Swahiba, Athuman Momba, Joseph Lusungu na Hamisi Kitambi.

Kipindi hicho Juwata jazz 'Wanamsondo ngoma' ilikuwa ikihudumiwa na wanamuziki takriban 28 wakiwemo na mafundi mitambo.

Tarehe 5.9.1991 bendi hii ilikuwa imekamilisha mazoezi ya nyimbo 9, na kuingia Studio za RTD kwa ajili ya kuzirekodi.





UK. 15

tanzaniabora @tanzaniabora @tanzaniabora

Tanzania BORA

# MICHEZO

IJUMAA Februari 07, 2025

Tovuti: www.tanzaniabora.co.tz

# Simba yaachia Pointi Manyara



NA MWANDISHI WETU

TIMU ya Simba hatimaye imeendelea kukaa nafasi ya pili katika msimamo wa Ligi Kuu Tanzania ya NBC baada ya jana kuambulia pointi moja katika mchezo wa ligi hiyo ilipocheza dhidi ya Fountain gate na kupata sare ya bao 1-1.

Licha ya kumiliki mchezo huo kwa vipindi vyote, Simba ilijikuta ikiambulia matokeo hayo baada ya kosa kubwa la kiungo wake Ladack Chasambi aliyejifunga baada ya kuurejesha mpira golini kwa shuti kali lililomshinda kipa Moussa Camara na kuukwamisha wavuni.

Bao la Simba lilifungwa na Leonel Ateba aliyewekewa

Inaendelea Uk.14

# AFCON YAZIDI KUPAMBA MOTO

NA MWANDISHI WETU

HOMA ya kufanyika kwa michuano ya AFCON katika nchi za Afrika Mashariki Uganda, Kenya na tanzania kunaendelea kupasua vichwa vya mashabiki wa soka, wanaojali tukio hilo kubwa la kihistoria.

Michuano hiyo itafanyika kwa ushirikiano wa nchi hizo ambazo ndiyo waandaji, huku kilka nchi ikieendelea na ujenzi pamoja na kufanya ukarabati wa miundombinu ili kuhakikisha michezo hiyo inafanyika bila vikwazo

Waziri anayeshugulikia michezo nchini Kenya Salim Mvurya amekuwa na kibarua kizoyto cha kusimamia maandalizi hayo usiku na mchana, huku Waziri mdogo katika Wizara ya Elimu na michezo anayeshugulikia eneo hilo nchini Uganda Peter Ogwang naye akieleza kujridhishwa mna maandeleo ya maandalizi ya michuano hiyo.

Nchini tanzania hivi karibuni Waziri Mkuu Kassim Majaliwa alisema Serikali imejipanga vyema kukamilisha maandalizi yote muhimu ikiwemo miundombinu kwa ajili ya Michuano ya Mpira wa Miguu kwa Nchi za Africa

Inaendelea Uk.14



# Yanga yashitukia zengwe Ligi Kuu

NA MWANDISHI WETU

AFISA Habari na Mawasiliano wa klabu ya Yanga Ali Kamwe amezitaka mamlaka zinazoshughulikia Ligi kuu Tanzania Bara, kufanya uchunguzi kwa baadhi ya michezo.

"Sio mara ya kwanza, ni mechi ya 10 mfululizo kila mechi kuna timu inajadiliwa kuhusu kupata magoli ya



kuzidi 'Offside' na Penalty za mchongo."

"Wenye mamlaka tunahitaji kusikia sauti zenu juu ya hiii nini kinachoendelea?.

"Haiwezekani timu moja tu iwe na matukio ya utata kwenye mechi zaidi ya 10." alisema kamwe bila kufafanua au kuitaja timu anayoituhumu kuhusika na matukio hayo.